

Vijenzi vya Uduara katika Sanaa za Maonyesho za Jamii ya Wangoni

Athumani S. Ponera na Martina Duwe
Chuo Kikuu cha Dodoma, Tanzania

Ikisiri

Makala haya yanafanua vijenzi vinavyounda na kuushikilia uduara kama kipengele kimojawapo maarufu cha falsafa ya Kiafrika. Hoja kuu ya makala ni kudhihirisha kuwapo kwa dhana ya uduara katika sanaa za maonyesho za jamii ya Wangoni. Makala haya ni sehemu tu ya matokeo ya uchunguzi mpana uliofanyika katika jamii ya Wangoni kuhusu dhana ya uduara. Data zilikusanywa kwa kutumia mbinu tatu ambazo ni usaili, ushuhudiaji wa utendekaji wa shughuli mbalimbali za kijamii, pamoja na udurusu wa kimaktaba. Makala yana sehemu tano. Sehemu ya kwanza ni utangulizi; ambapo dhana za msingi zinazoyajenga makala zimedokezwa. Sehemu ya pili inafanua vijenzi vya dhana ya uduara. Sehemu ya tatu inahusu tija za dhana ya uduara. Sehemu ya nne ni hitimisho, na sehemu ya tano ni marejleo. Kwa ujumla, mjadala wetu umeonyesha kuwa sehemu kubwa ya matukio, matendo na vitu vinavyohusiana na Wangoni hufanywa au kuundwa kwa umbo la duara. Katika makala haya, matukio, matendo na vitu hivyo, vimeelezwa kama ni vijenzi. Vijenzi hivyo ni vitatu. Navyo ni: uchezaji wa ngoma, michezo ya watoto, pamoja na ujumi wao unaojidhihirisha kupitia vifaa mbalimbali vya kutekelezea sanaa za maonyesho.

Maneno Muhimu: Uduara, Vijenzi vya Uduara, Falsafa ya Kiafrika

Utangulizi

Makala haya yanajadili uduara unavyojitokeza katika sanaa za maonyesho za Wangoni. TUKI (2013) inasema kuwa duara au duwara ni umbo la mviringo au mzunguko. Hivyo basi, uduara ni hali ya kitu au jambo kuwa au kufanyika katika umbo la mviringo. Hali hii huweza kujitokeza katika maeneo, mambo na vitu mbalimbali. Kwa mfano, chombo huweza kuwa na umbo la duara na shughuli mbalimbali za kijamii na/au za kiuchumi pia huweza kufanywa kwa umbo la duara. Vilevile, mchezo huweza kucheza kwa umbo la uduara. Uduara unajadiliwa humu kama kipengele kimojawapo cha kifalsafa. Dhana ya falsafa huelezwa kwa kujielekeza katika mielekeo ya umbo-nyenzo na umbo-nadharia. Mtaalamu mmojawapo anayeielezea falsafa kwa mwelekeo

wa umbo-nyenzo ni Mihanjo (2009) ambaye ananukuliwa na Chuachua (2016:4) akieleza kuwa: “Falsafa ni tochi ya kumulikia matukio. Bila ya kuwa na tochi, huwezi kuyamulika matukio. Falsafa inatoa dira ya ndani ya kuyaelewa maudhui ya matukio.” Kwa mwelekeo wa kiumbo-nadharia, falsafa huonwa kama taaluma au uga unaofumbata ‘ukweli’ unaofafanua kipengele au vipengele fulani vya maisha. Kwa mwelekeo wa umbo-nyenzo, falsafa huelezwa kama chombo cha kuchunguza undani na mienendo ya mtu na/au jamii. Fasili mojawapo inayoyakinisha mwelekeo huu ni ile ya Bakhresa (1992) anayeitazama falsafa kama elimu ya busara, maarifa na hekima. Pamoja na kufanyiwa sana kazi, uga huu wa falsafa, chambilecho Chuachua (2010 na 2016), utaendelea kupata mielekeo mipya ya kiufafanuzi kadri unavyoendelea kushughulikiwa.

Uduara katika Sanaa za Maonyesho za Jamii ya Wangoni

Tumedokeza hapo juu kuwa uduara unajadiliwa kama kipengele kimojawapo cha falsafa ya Kiafrika. Falsafa ya Kiafrika ni fikra, busara na elimu (maarifa na ujuzi) kuhusiana na maisha ya Waafrika. Kumekuwapo na maoni tofauti kuhusu kuwapo au kutokuwapo kwa falsafa ya Kiafrika. Kuwapo kwa falsafa ya Kiafrika kumethibitishwa na wanazuoni kama vile Tempels (1959), Mbiti (1969), Sengo (1995), Chuachua (2010, 2016) na Simchimba (2012). Wataalamu hawa wametafiti na kuonesha kuwa Waafrika wana falsafa yao ambayo hujidhihirisha kupitia kwa matendo, sanaa, na utamaduni wao (lugha, mila, desturi na kunga zao). Mdhihiriko huo huwa tofauti na unavyodhihirika katika jamii nyingine. Vipengele vinavyojichomoza sana katika falsafa ya Kiafrika (na kudhihirika kwa namna yenye upekee), ni pamoja na matambiko, uchawi, uganga, mapenzi na ndoa, kifo na uhai, umoja au upamoja, uzazi, utoaji wa majina, pamoja na uduara (Chuachua, 2010 na 2016; Faustine, 2017). Waafrika huviamini, kuviegemea, na kuvitumia vipengele hivi katika uendeshaji wa maisha yao ya kila siku; hii ndiyo falsafa yao. Kwa hiyo basi, falsafa ya Kiafrika haiwezi kutenganishwa na maisha halisi ya Waafrika. Hata hivyo, ni vema ieleweke hapa kuwa dhana ya U-Afrika ni pana na tata. Ni dhana pana kwa sababu inajumuisha jamii nyingi; na, ni dhana tata kwa sababu jamii hizo hutofautiana katika vipengele mbalimbali kama vile rangi, lugha na taratibu nyingine za kimaisha. Katika kujadili masuala mbalimbali yaihusuyo Afrika (kama vile isimu, historia, utamaduni na sanaa), bara hili hutazamwa kwa kuyaangazia maeneo ya kikanda. Ponera (2014) anazidokeza kanda zifuatazo: Kanda ya Kaskazini (Kanda ya Uarabuni), Kanda ya Magharibi, Kanda ya Pembe ya Afrika, pamoja na Kanda ya Kusini mwa Sahara (yakiwemo maeneo ya Afrika Mashariki, Kati na Kusini). Kwa kuzingatia hilo, makala haya yanaichukulia dhana ya U-Afrika kwa kuiegemeza katika eneo lote la Afrika lililo nje ya Kanda za Kaskazini na Kanda ya Pembe ya Afrika. Tunaamini kuwa jamii za eneo hili zinaendana kwa vipengele vingi vya kifalsafa.

Wangoni ni mojawapo ya jamii nyingi zinazopatikana katika eneo hili, hususani nchini Tanzania. Dhana ya Wangoni, katika makala haya, inamaanisha kundi la watu wanaozungumza lugha ya Kingoni na kuishi kwa kuongozwa na taratibu maalum zinazopatikana katika kundi hilo. Asili ya kundi hili ni nchi ya Afrika ya Kusini, katika

eneo la Kwa Zulu-Natal. Wangoni walianza kuikimbia nchi yao ya Afrika ya Kusini na kwenda kuishi katika nchi nyingine za Afrika kama vile Tanzania, Malawi, Msumbiji na Zambia mnamo Karne ya Kumi na Tisa kutokana na ongezeko la watu katika nchi hiyo lililosababisha vita vya kugombea rasilimali mbalimbali, ikiwemo ardhi (Ebner, 2009). Nchini Tanzania, jamii hii iliweka makazi yake katika mkoa wa Ruvuma ikijumuisha jamii ndogondogo tatu. Jamii hizo ni Wamatengo wanaopatikana kwa wingi wilayani Mbinga, Wandendeule wanaopatikana wilayani Namtumbo, pamoja na Wangoni wanaopatikana kwa wingi wilayani Songea (Millinga, 2016). Jamii ya Wangoni ndiyo inayoegemewa na makala haya kufafanua vijenzi vya uduara vinavyojitokeza katika sanaa zao za maonyesho.

Sanaa za maonyesho hujumuisha vipengele vya kiutendaji ambavyo hukitwa katika unenaji na uchezaji. Miongoni mwa vipengele hivyo ni ushairi wa majibizano, ngoma za kienyeji, muziki na maonyesho ya jukwaani. Wahusika wa sanaa za maonyesho, kwa kiasi kikubwa huwa watu; na, kwa kiasi kidogo, hutumia vikaragosi. Mfano maarufu wa sanaa za maonyesho zitumiazo vikaragosi, hususani katika jamii ya Wangoni ni mchezo wa *ngongoti*. Huu ni mchezo unaotumia kikaragosi cha fito/miti. Kikaragosi hicho huvishwa maleba na kuchezesha kwa namna tofauti ili kuakisi lengo la mchezeshaji au tukio husika. Mizizi ya sanaa za maonyesho hujitokeza katika vipengele vya sanaa-jadi kama vile utongoaji wa simulizi mbalimbali (kwa mfano, usimulizi wa visasili unaoendana na utendaji). Pia, hujitokeza katika shughuli za kijamii (kama vile sherehe [za kuzaliwa mtoto, za mavuno, za ndoa na za jando/unyago], matambiko na misiba), shughuli za kidini, pamoja na (Mbogo, 1993; Banham, 2004). Conteh-Morgan (2004) anaongezea kuwa, kwa jumla, vipengele hivi vyote sanaa za maonyesho huangukia katika makundi makubwa mawili: kundi la kuburudisha na kundi la kuabudu. Sanaa za maonyesho za kundi la kuabudu hujitokeza katika matukio ya tiba (uganga), maombezi ya maradhi na/au mabaa kama vile mvua na njaa. Makala haya yanavifafanua vijenzi vitatu vya uduara. Navyo ni: uchezaji wa ngoma, michezo ya watoto na ujumi (maumbo ya vifaa). Ufuatao ni ufafanuzi wa vijenzi hivyo pamoja na kuonyesha mdhihiriko wake katika jamii ya Wangoni:

Uchezaji wa Ngoma

Ngoma ni mojawapo ya fani za Fasihi Nenwa¹ ya Waafrika. Wangoni, kama jamii mojawapo ya Kiafrika, nao wana ngoma mbalimbali. Makala haya yanafafanua ngoma sita ambazo zimetamalaki katika jamii hiyo. Ngoma hizo ni *Chihoda*, *Madogoli*,

¹ Dhana ya Fasihi Nenwa tunaitumia kumaanisha kazi za kisanaa zinazowasilishwa kupitia unenaji (uneni); huku tukiweka msisitizo kuhusu kuwapo kwa tofauti kati ya Fasihi Nenwa (*Oral Literature*) na Fasihi Simulizi (*Narrative Literature*). Makala haya yanaichukulia Fasihi Nenwa kama dhana kuu, na Fasihi Simulizi kama dhana bebwa inayopatikana ndani ya Fasihi Nenwa (Ponera, 2014).

Lizombe, Chomanga, Beta, na Mkwajungoma. Yafuatayo ni maelezo kuhusu ngoma hizo na uchezaji wake: Ngoma ya *Chihoda* (pia huitwa *Kioda*) huchezwa na akina mama wakati wa sherehe, sikukuu au kwenye tukio la kumkaribisha mgeni wa kiserikali au wa kidini anayetembelea katika jamii ya Wangoni. Wachezaji hujifunga nguo kiunoni. Wengine hufunga vitambaa mikononi au vichwani. Wengine huvaa kofia au miwani na kushika tochi mkono wa kushoto. Wakati mwingine, kanga wanazofunga viunoni huwa zinafanana. Pia, huweza kushika vifaa kama vile ungo, kapu lenye unga, ndoo yenye maji na chungu. Vifaa hivyo hushikwa kwa shabaha mbili: mosi, kuakisi uhalisi wa shughuli na majukumu ya mwanamke. Pili, hutumika kama zana zinazorahisisha kufikisha ujumbe kulingana na muktadha wa tukio linalohusika na ngoma hiyo. Hucheza kwa namna ya kuzungusha viuno vyao kwa madaha, na kwa minenguo inayolingana huku wakiimba nyimbo na kupiga filimbi pale inapobidi. Hucheza wakiwa katika duara; wote kwa pamoja hujongea upande mmoja kwa kufuata mapigo ya ngoma. Mjongeo huo huwafanya wawazunguke wapiga ngoma, ambao mara nyingi huwa wanaume. Watazamaji nao husimama kwa umbo la duara wakiwazunguka wachezaji.

Ngoma ya *Madogoli* huchezwa na wanawake au wanaume kwa namna ya duara. Wachezaji hucheza na kuimba huku wakiwazunguka wapiga ngoma. Watazamaji nao huwazunguka wachezaji kwa lengo la kuwatazama vizuri wanavyocheza na kusikiliza vema maudhui yaliyomo katika nyimbo zinazoimbwa. Nyimbo hizo huwa na maudhui tofauti kulingana na tukio au wahusika wa tukio hilo. Kwa mfano, kama wanamwimbia mwali, basi maudhui huweza kuwa ya kuonya au kuasa, kuadilisha na kuelimisha.

Lizombe pia ni ngoma inayochezwa wakati wa matukio mbalimbali katika jamii ya Wangoni kama vile sherehe na sikukuu. Hii ni ngoma maarufu zaidi inayotumika kuitambulisha jamii ya Wangoni nje ya mipaka yake. Katika kucheza ngoma hii, wachezaji humzunguka mpiga ngoma na kutengeneza umbo la duara. Wachezaji hujifunga kanga mbili, moja hujifunga kwa namna ya kujitandaza kuanzia viunoni ikishuka chini, na nyingine hukunjwa na kuzungusha viunoni mwao. Miguuni hujifunga njuga zenye kutoa sauti kulingana na mtikisiko wa miguu yao. *Lizombe* huchezwa na watu wa jinsi zote, wanawake na wanaume. Kwa kawaida, ngoma hii huwa na nyimbo fupifupi sana. Wachezaji huziimba kwa namna ya kupokezana. Ngoma hupigwa kwa namna ya mkato mkato, yaani hupigwa na kusitishwa ili kumpa nafasi kiongozi atumbuize; na anapomaliza, wachezaji wote humpokea kuimba sambamba na kucheza.

Ngoma ya *Chomanga* huchezwa na akina mama huku wakiwazunguka wapiga ngoma. Uchezaji wao ni wa umbo la duara. Wanapocheza ngoma hii, huimba nyimbo zenye ujumbe mahsusi kulingana na tukio husika huku wakipiga makofi yanayoenda sambamba na wimbo unaoimbwa. Makofi hayo hupigwa kiufundi bila kutofautiana. Pia, wachezaji hupeana zamu ya kila mmoja kuingia ndani (katikati) ya duara kucheza kwa madaha kwa kutumia minenguo ya kipekee, kisha kurudi katika sehemu aliyotoka. Uchezaji huu wa kuingia ndani na kutoka ni sehemu ya upekee unaojitofautisha na uchezaji wa ngoma nyingine za jamii ya Wangoni. Wanapocheza kwa kuzunguka,

huhakikisha hawaharibu duara lao kwa lengo la kupeana nafasi wakati wa kucheza. Watazamaji nao huwazunguka wachezaji huku wakiwashangilia. Ngoma ya *Betahutokana* na kifaa maalumu kinachotumika kupigia ngoma hii kiitwacho *mbeta*. Hiki ni kipande cha mwanzini kinachounganishwa na waya mwembamba. Ngoma hii inapopigwa, hutoa mlio kulingana na mahitaji ya mpigaji. Vifaa vingine vinavyotumika katika ngoma hii ni ngoma kubwa na ngoma ndogondogo, filimbi, jembe na ufito wa chuma unaotumika katika kukwaruza au kusugua *mbeta* ili kutoa sauti maalumu. *Betahuchezwa* na watu wazima wa jinsi zote wakiwa wamejifunga kanga viunoni. Kanga hizo huweza kuwa sare kwa wote au kwa makundi ya watu (kama vile watatu-watatu au wanne-wanne). Pia, kiongozi wao huweza kuvaa ngozi ya wanyama kama sehemu ya upekee wa kintindo wa ngoma hiyo. Wanapocheza, husimama katika umbo la duara na hucheza kwa umakini bila kuharibu duara hilo. Watazamaji nao husimama kwa kuwazunguka wachezaji wakiwashangilia na kusikiliza maudhui ya nyimbo zao. Kama ilivyo kwa ngoma nyingine, ngoma ya *beta* huchezwa kwenye sherehe mbalimbali, sikukuu au kama kuna ujio wa viongozi maalumu katika jamii yao.

Ngoma ya *Mkwajungoma* huchezwa pia kwa wachezaji kuwazunguka wapiga ala za ngoma bila kuharibu duara hilo. Kifaa ambacho ni kiungo muhimu katika ngoma hii ni marimba. Wakati wa kucheza, watazamaji husimama pembeni kwa umbo la duara. Tumeleza kuwa ngoma zote za jamii ya Wangoni huchezwa katika muundo wa umbo la duara. Kwa jumla, uchezaji wa ngoma hizo hudhihirisha kuwapo kwa thamani ya dhana ya uduara kupitia namna au muundo wa uchezaji. Hali hii ya ngoma za jamii hii kucheza katika umbo la duara lina upekee. Upekee huo inajidhihirisha kwa wazi zaidi inapolinganishwa na uchezaji wa ngoma za jamii nyingine za jirani kama vile Wayao (wa wilaya ya Tunduru) na Wamatengo (wa wilaya ya Mbinga). Kwa mfano, Wayao wanayo ngoma yao maarufu iitwayo *Likachunje* ambayo wachezaji wake hujipanga katika mistari miwili inayotazamana. Kwa upande wao, Wamatengo wana ngoma ya *Mganda* ambayo wachezaji wake hujipanga katika mistari miwili au zaidi (wote wakitazama upande mmoja). Kiango (1973) anathibitisha jambo hili la kutamalaki kwa uduara katika ngoma za Waafrika kwa kusema kuwa, kwa Waafrika, toka zamani ngoma ilichezwa na kila aliyehitaji kucheza. Ngoma hiyo ilichezwa kwa mzunguko; na watazamaji waliwazunguka wachezaji hao kwa lengo la kila mmoja kuweza kuona vema kinachotendeka. Hii ni wazi kuwa, tangu zamani, Waafrika walipenda kutenda jambo kwa umbo la duara kama inavyojidhihirisha katika jamii ya Wangoni.

Michezo ya Watoto

Kucheza ni sehemu ya kazi na furaha ya watoto. Watoto wa jamii ya Wangoni hushiriki katika michezo mbalimbali kwa ushirikiano. Makala haya yanafafanua michezo ya *TindilaTindila*, *Ukuti Ukuti*, *Dosi Njelele*, *Ninamtaka Rafiki*, *Kadunda Kahikili*, na *Kificho*. Yafuatayo ni maelezo kuhusu uchezaji wa michezo hiyo:

Mchezo wa *TindilaTindila* umekitwa katika kitenzi cha Kingoni *tindila* chenye maana ya zunguka. Watoto wa idadi yoyote hujipanga katika umbali wa hatua moja au mbili (kutoka mtoto mmoja hadi mwingine); hushikana mikono na kuungana kiasi cha kutengeneza umbo la duara. Kisha, huanza kuimba huku wakitengeneza mjongo wa

uelekeo mmoja (aghalabu, hujongea kuelekea kulia). Mchezo huchezwa kwa kuhusisha matendo manne: kuunda duara kupitia kushikana mikono, kuimba, kujongea upande mmoja kwa hatua maalum zinazoendana na mapigo ya wimbo, pamoja na kuchuchumaa na kusimama kwa kufuata mapigo ya wimbo na mjongeo. Wimbo uimbwao katika mchezo huu huakisi jina la mchezo wenyewe, yaani *Tindila Tindila*. Wimbo wenyewe ni huu:

Tindila tindila tama pae ahee ahee tama pae!
Tindila tindila tama pae ahee ahee tama pae!
Tindila tindila tama pae ahee ahee tama pae!
Tindila tindila tama pae ahee ahee tama pae!
Tindila tindila tama pae ahee ahee tama pae!
Tindila tindila tama pae ahee ahee tama pae!
Tindila tindila tama pae ahee ahee tama pae!

Tafsiri:

Zunguka zunguka kaa chini ahee ahee kaa chini!
Zunguka zunguka kaa chini ahee ahee kaa chini!
Zunguka zunguka kaa chini ahee ahee kaa chini!
Zunguka zunguka kaa chini ahee ahee kaa chini!
Zunguka zunguka kaa chini ahee ahee kaa chini!
Zunguka zunguka kaa chini ahee ahee kaa chini!
Zunguka zunguka kaa chini ahee ahee kaa chini!

Wimbo huu ndio msingi wa mchezo wa *Tindila Tindila*. Dhana ya kuzunguka (*kutindila*) hujengwa na kitendo cha wachezaji wote kuendelea kujongea kwa kuruka wakielekea upande mmoja wakiwa wameshikana na kuunda duara. Huendelea kucheza na kuimba bila kuachanisha mikono wala kuharibu duara. Atakayeonekana amechoka, hutolewa nje na mwingine huingia mahali pake. Atakayeweza kucheza mpaka mwisho bila kutolewa nje, basi huyo ni mshindi wa mchezo husika. Watoto wengine husimama nje kwa umbo la duara. Hawa huwasaidia wachezao kuimba wimbo. Pia, huangalia nani anakosea au amechoka ili atolewe nje ya mchezo. Mchezo huu huchezwa na watoto wanapokuwa nyumbani au katika mazingira ya shuleni.

Mchezo wa *TindilaTindila* tulioufafanua hapo juu unalandana sana katika muundo wa uchezaji na mchezo mwingine unaoitwa *Ukuti Ukuti*. Mchezo huu pia huchezwa na watoto wakiwakatika umbo la duara. Hushikana mikono na kuzunguka bila kuachana. Wachezaji wake huweza kuwa watoto wa kike na wa kiume. Wanapocheza, huimba wimbo wa *Ukuti Ukuti* ambao huanzishwa na mmoja wao. Kwa hiyo, wimbo huo ndio unaoushikilia mchezo. Ifuatayo ni mishororo ya wimbo huo:

Mwanzishaji: Ukuti ukuti!
Kiitikio: Wa nazi wa nazi!
Mwanzishaji: Mwenzetu mwenzetu!
Kiitikio: Kagongwa kagongwa!
Mwanzishaji: Na nini na nini!

Kiitikio: Na gari na gari!

Wote: Tumpeleke Peramiho, atakayekataa shauri yake, yesa yesa yesa yeee!
yesa tena, yesa yesa yesa yeee.

Wanapoimba, huanza kujongea taratibu kuelekea upande mmoja, huku kiongozi wao akianzisha wimbo na wao kuitikia. Wanapofika sehemu ya kuimba wote ambayo ni “tumpeleke Peramiho atakayekataa shauri yake yesa yesa yesa yeee, yesa tena yesa yesa yesa yeee,” huongeza kasi ya kukimbia huku wakichuchumaa na kusimama harakaharaka kwa kufuata mapigo maalum ya hatua. Neno Peramiho linalotajwa katika kibwagizo cha wimbo huu ni jina la hospitali kubwa iliyopo wilaya ya Songea Vijijini. Kwa hiyo, muundo wa uchezaji wa mchezo wa *Ukuti Ukuti* pamoja na ule wa *Tindila Tindila* inatudhihirishia kuwapo kwa dhana ya uduara katika michezo ya watoto wa jamii ya Wangoni. Mchezo wa *Dosi Njelele* huchezwa na watoto wakiwa katika kundi la watatu na kuendelea. Mara nyingi, mchezo huu huchezwa nyakati za jioni watoto wakiwa katika viunga vya majumbani mwao. Wachezaji hukaa ardhini na kunyoosha miguu au mikono yao kuelekea katikati aliko kiongozi wao. Baada ya kuketi, kiongozi hunzisha wimbo. Yafuatayo ni maneno ya wimbo huo:

Dosi njelele dosi njelele!

Dosi njelele dosi njelele!

Dosi njelele dosi njelele!

Dosi njelele dosi njelele!

Tihamba Kulitanda kumbeleweta kulya mkati wa Nyanja!

Wakapilika sekendu kanisani ngolimbe!

Kamoja, kambili tandika mpasa kumagulu de!

Delula kumtuma kumanji de!

Tafsiri:

Dosi njelele dosi njelele!

Dosi njelele dosi njelele!

Dosi njelele dosi njelele!

Dosi njelele dosi njelele!

Twende bwawani kula mkate wa Nyasa!

Ukisikia kengele ujue imelia kanisani!

Moja mbili utandike mkeka na unyoshe miguu!

Utakapokunjua miguu safari kuteka maji!

Kama tulivyoeleza nafasi ya wimbo katika mchezo uliopita, wimbo huu pia ndio msingi wa mchezo wa *Dosi Njelele*. Kifungu cha ‘Dosi njelele’ ni msemu unaomaanisha ‘kitu au jambo laini’ au ‘hali ya unyoronyoro’. Wimbo unapoanza kuimbwa, kiongozi huanza kushika mikono au miguu mmojammoja iliyonyoosha kumwelekea yeye. Hufanya hivyo kwa kumgeukia kila mchezaji bila kumruka yeyote. Huendelea kufanya hivyo mpaka inapofika mwisho wa wimbo. Aliyeguswa pale wimbo unapokomea huitwa mtu laini au mchawi wa mchezo (dosi njelele); hivyo, hutakiwa kutoka nje ya mchezo. Kitendo hiki cha kutolewa nje ya mchezo

kinasawiriwa na kifungu cha mshororo wa mwisho kinachohusu ‘safari ya kwenda kuteka maji’. Wimbo huanza tena, na kiongozi huendelea na kitendo cha kugusa mguu wa kila mmoja mpaka wimbo unapoisha. Mchezaji wa mwisho kuguswa katika awamu husika ya uimbaji huendelea kutolewa nje ya mchezo mpaka apatikanapomshindi mmoja. Hivyo, tumeona kuwa msingi wa uchezaji wa mchezo huu — kuanzia mkao wa wachezaji pamoja na kitendo cha kiongozi kugusa miguu ya wachezaji kwa namna ya kuwazungukia — inaakisi hali ya uduara. Mchezo wa *Ninamtaka Rafiki* hucheza na watoto wanapokuwa shuleni au nyumbani. Wanapocheza, hushikana mikono yao huku wakiwa katika umbo la duara. Wakiwa katika umbo hilo, huanza kutembea kwa hatua za taratibu na zinazofanana kuelekea upande mmoja huku mmoja wao akianzisha wimbo wa *Ninamtaka Rafiki*, na wengine huitikia. Ifuatayo ni mishororo ya wimbo huo:

Mwanzishaji: Ninamtaka rafiki iyoyoyoyooo!
Kiitikio: Rafiki yako naani iyoyoyoyooo!
Mwanzishaji: Rafiki yangu Mage iyoyoyoyooo!
Wote: Naye Mage cheza naye iyoyo bampingi!
Kama hutaki useme utolewe, x2.

Anayeanzisha wimbo ndiye mwenye jukumu la kutaja jina la rafiki anayemtaka ili aingie ndani au katikati ya duara aweze kucheza naye. Mmoja akishachaguliwa, wengine hucheza kwa kuzunguka haraka haraka huku wakiendelea kuimba kwa pamoja. Anayetajwa jina lake huingia ndani ya umbo-duara waliloliunda, huku wengine wakiwa wanaendelea kuimba wimbo na kushiriki katika kucheza. Mtoto anayechaguliwa hujisikia furaha kwa sababu anaamini kuwa wenzake wanampenda. Huendelea kubadilishana katika kumchagua rafiki mpaka wote watakapomalizika au kuchoka kucheza mchezo huu. Hali hii ya kucheza wakiwa katika umbo la duara hudhihirisha kuwapo kwa dhana ya uduara pamoja na thamani yake katika jamii yao. Mchezo mwingine unaitwa *Kadunda Kahikili*. Neno *kadundamaana* yake ni mlima, na *Kahikili* maana yake ni umefika. Huu ni mchezo unaochezwa na watoto wa kike na wa kiume; aghalabu, hutakiwa kuwa wengi — kuanzia watoto wanane na kuendelea. Mchezo huanza kwa mtoto mmoja kuinama. Kisha, mwingine hufuatia nyuma yake na kushikilia shati au gauni la yule wa mbele yake kwa umakini bila kuachilia huku akiwa amefumba macho. Wengine nao hufuatia na kufanya hivyo (kuinama, kushika nguo ya aliye mbele, na kufumba macho). Hujipanga hivyo na kutengeneza namna fulani ya duara. Huwa haliwi duara kamili kwa sababu huachwa upenyu kati ya mchezaji aliyeanzisha na wa mwisho. Mchezaji anayeanzisha duara hatakiwi kushika nguo ya mchezaji yeyote. Hivyo, yeye (mtoto aliyeanzisha duara) ndiye huongoza safari wakati wale wengine hawajui waendako kutokana na kufumba macho yao. Mwongozaji huwatembeza wenzake katika namna ya kuzunguka; huwazungusha wenzake waliofumba macho mara kadhaa. Watembeapo wakiwa katika umbo hilo la duara, huimba wimbo. Wimbo wenyewe ni huu:

Mwanzishaji: *Kadunda Kahikili*.

Kiitikio: *Kakona*.

Mwanzishaji: *Kadunda Kahikili?*

Kiitikio: *Kakona*.

Mwanzishaji: *Kadunda Kahikili?*

Kiitikio: *Kakona*.

Mwanzishaji: *Kadunda Kahikili?*

Kiitikio: *Kakona*.

Tafsiri:

Mwanzishaji: Mlima umefika?

Kiitikio: Bado.

Mwanzishaji: Mlima umefika?

Kiitikio: bado.

Mwanzishaji: Mlima umefika?

Kiitikio: bado.

Mwanzishaji: Mlima umefika?

Kiitikio: Bado.

Waimbaji huendelea kuzunguka huku wakiimba wimbo huu. Kiongozi wao anapoona kuwa wamezunguka vya kutosha, husimama na huwaambia wenzake kuwa *kadunda kahikili*. Hivyo basi, huwaambia wafumbue macho yao na kisha huwauliza maswali kama vile ‘tumezunguka mara ngapi?’ Au ‘tumeimba wimbo mara ngapi?’. Nao hutakiwa kujibu maswali kwa pamoja. Anayeonekana amekosea, huadhibiwa kwa kutolewa nje; na hutakiwa kuwaangalia wenzake kama wanafumba macho wakati wa kucheza mchezo kwa mara nyingine. Dhima hii ya ki-adhabu huwa nyepesi kufanywa na yule aliyeadhibiwa kutokana na wachezaji kuwa katika umbo hilo la duara. Hivyo, huweza kupepesa macho ya kiukaguzi kwa haraka kwa washiriki wote wa mchezo. Kwa kawaida, wachezaji huwa hawapendi kuadhibiwa kutokana na kukosea, hivyo, huwa hucheza na kuimba huku wakiwa makini kuhesabu mizunguko na idadi ya marudio ya wimbo.

Pia, kuna mchezo wa *Kificho*. Mchezo huu huchezwa kwa kukusanya mchanga na kutengeneza mafungumafungu. Mafungu hayo huwa kati ya matano hadi kumi; na hupanngwa katika umbo la duara. Fungu moja hukadiriwa kuwa na mchanga wenye ujazo wa kati ya kilogramu moja hadi mbili. Watoto hukaa pembeni ya mchanga kwa kufuatisha umbo hilo la duara. Mmoja kati yao huanza kucheza kwa kushika kijiti au jiwe dogo lisiloweza kuonekana kwa urahisi. Huchomekachomeka katika mafungu hayo ya mchanga kwa haraka haraka. Huachilia jiwe au kijiti hicho katika fungu mojawapo. Kwenye kila fungu la mchanga anapochomeka huhakikisha amelisawazisha vizuri ili kuwapa wenzake kazi ya kukitafuta kijiti au jiwe hilo haraka haraka. Anayewahi kukiona, huwa ni zamu yake kucheza. Naye hufanya vivyo hivyo, na wenzake hutafuta kijiti au jiwe hilo. Huendelea hivyo mpaka wanapokuwa wote wamemaliza kucheza au wanapochoka. Watoto hupenda kucheza mchezo huu wakiwa

katika mazingira ya nyumbani au shuleni. Michezo yote hii huchezwa huku wachezaji wakiwa katika umbo la duara. Kwa jumla, utendekaji wa michezo yote hii ya watoto kwa namna ya duara hudhihirisha kuwa uduara, kama kipengele kimojawapo cha falsafa ya Kiafrika, upo hai katika jamii ya Wangoni, na Waafrika kwa upana wake.

Ujumi wa Vifaa vya Kutendea Sanaa za Maonyesho

Ujumi ni taaluma ya thamani ya uzuri na/au ubaya wa kitu/jambo/hali. Wangoni wanayo miegamo yao ya kihisia, kiidili na kimatumizi kuhusu thamani ya uzuri na/au ubaya wa mambo yanayowazunguka. Idili ni vipimo au vigezo vya kupimia na kuhakikia kuwapo kwa uzuri au/na ubaya katika hali, jambo au kitu fulani (Ponera, 2014). Kijenzi hiki cha uduara katika jamii ya Wangoni kinafafanuliwa kwa kutumia maumbo ya vifaa vinavyotumika katika utendaji wa vipengele vya sanaa za maonyesho.

Kuhusu kipengele cha vifaa vya kijadi vinavyotengenezwa na kutumiwa na Wangoni katika maisha yao ya kila siku, sehemu kubwa ya vifaa hivyo huwa katika umbo la duara. Vifaa hivyo hutengenezwa kwa kutumia udongo, pamoja na mimea kama vile nyasi, mianzi, matete na miti. Mifano ya vifaa hivyo ni kama vile *chijomela*, *vinu*, *chifuru* (mtungi), chungu cha mboga, *chiheneku*, pamojana nyungo. *Chijomela* ni chombo chenye umbo la mviringo kinachotengenezwa kwa nyasi zinazoota katika mazingira ya Ungonini. Kwa Kingoni, kili hizo zinaitwa *malulu*. *Chiheneku* ni kifaa kinachofanana na ungo, lakini ni kidogo kwa umbo na hutengenezwa kwa mianzi inayopatikana katika mazingira yao.

Kwa jumla, vifaa vyote hivi huwa katika umbo la duara. Vifaa hivi hutumika katika matukio ya sanaa za maonyesho kama vile matambiko, sherehe, na misiba. Katika matambiko, mathalani, matumizi ya vifaa kama vile *chifuru* na nyungo ni ya lazima. Hapa, hoja ya makala ni kwamba, ingewezekana kabisa vifaa hivi vikatengenezwa kwa kuakisi maumbo mengine kama vile pembe tatu au pembenne bila kubadili maana wala hadhi yake. Bali, hutengenezwa katika umbo au sura hiyo ya uduarakutokana na mazoea ambayo wanajamii wanayo. Mazoea hayo hupokezanwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Na, hivyo, kukiariidhi vema kipengele cha uduara katika jamii ya Kingoni na ya Kiafrika kwa ujumla.

Tija za Dhana ya Uduara kwa Jamii ya Wangoni

Utendekaji wa mambo kwa namna ya uduara katika jamii ya Wangoni una tija kadhaa kwa wanajamii. Ufuatao ni ufafanuzi wa tija hizo:

Mosi, dhana ya uduara huleta na kudumisha ushirikiano miongoni mwa wanajamii. Ushiriki wa shughuli za sanaa za maonyesho kama vile ngoma na michezo ya watoto kama ilivyodokezwa hapo juu huimarisha suala la upamoja miongoni mwa wanajamii. Uduara, kama kipengele cha falsafa ya Kiafrika, husaidia kuleta umoja na mshikamano kwa watoto wa jamii ya Wangoni. Uchunguzi umebaini kuwa watoto wa Kingoni hucheza michezo yao mbalimbali kwa umbo la uduara kwa lengo la kuruhusu kila mmoja anayehitaji kushiriki kucheza mchezo huo kuweza kucheza na wenzake kwa

pamoja. Kwa mfano, mchezo wa *Tindila tindila* ambao huchezwa kwa sura ya duara, haubagui rika wala jinsi ya mtoto. Kila anayehitaji kucheza, hucheza na wenzake kwa kushikana mikono. Wanapoimba kwa pamoja nyimbo mbalimbali katika umbo la uduara, hujenga ushirikiano miongoni mwao.

Kipengele cha uduara pia huleta tija katika matukio ya nje ya shughuli za sanaa za maonyesho. Mathalani, watoto wanapokula kwa umbo la duara, hujifunza kuthaminiana wenyewe kwa wenyewe na kuondokana na tabia ya ubinafsi au uchoyo. Kwa sababu wanapokula kwa duara, kila mmoja humtazama mwenzake; hivyo, ni rahisi kugundua anayekosekana, hatimaye, kusaka mahali alipoenda. Kama haonekani kabisa, watoto wengine humfuata kwa majirani au huamua kumhifadhia chakula. Pia, dhana ya uduara ina tija ya kufunza watoto na kuweza kubaini kuwa hata kama chakula ni kingi au kidogo ni vema kiliwe kwa wote na kwa usawa. Kwa hiyo, kila mmoja humfikiria mwenzake bila kuonyesha tabia ya ubinafsi; tofauti na kila mmoja akila katika sahani yake, ambapo mtoto anajifunza tabia ya ubinafsi na siyo upamoja kama falsafa ya Waafrika inavyotaka. Tija hii ya kuthaminiana na kujaliana hujitokeza pia katika michezo tuliyoielezea katika sehemu iliyopita. Kwa hiyo, dhana ya uduara ina dhima kubwa ya kuwajengea watoto misingi ya kuishi kwa ushirikiano bila ubaguzi miongoni mwao.

Pili, dhana ya uduara kwa jamii ya Wangoni ina tija ya kutunza siri kuhusu jambo fulani linalotendwa au kujadiliwa ambalo ni muhimu na halipaswi kuingiliwa na wengine. Kwa mfano, katika michezo iliyoenezwa hapo juu, ni wazi kuwa hali ya kucheza katika duara hutengeneza mazingira fulani ya urasmi ambayo hayawezi kuingiliwa kirahisi na mtoto mwingine asiyehitaji kucheza mchezo husika. Hii ni tofauti kama ingekuwa inachezwa katika umbo la mstari au mistari minyoofu.

Hitimisho

Makala yamefafanua vijenzi vinavyodhihirisha kuwapo kwa dhana ya uduara katika jamii ya Wangoni. Kijenzi kimojawapo kilichojadiliwa ni uchezaji wa ngoma. Hapa tumefafanua uchezaji wa ngoma sita ambazo ni *Chihoda*, *Madogoli*, *Lizombe*, *Chomanga*, *Beta*, na *Mkwajungoma*. Kijenzi kingine ni michezo ya watoto. Hapa tumefafanua michezo ya: *TindilaTindila*, *Ukuti Ukuti*, *Dosi Njelele*, *Ninamtaka Rafiki*, *Kadunda Kahikili*, pamoja na *Kificho*. Kijenzi cha tatu ni ujumi wa vifaa vya kutekelezea sanaa za maonyesho ya Wangoni. Sura ya jumla ya makala imedhihirisha kuwapo kwa dhana ya uduara katika utendekaji wa sanaa za maonyesho za jamii ya Wangoni. Uduara huo umeonekana kuwa na tija kama vile kuimarisha umoja na mshikamano, kutengeneza mazingira ya u-faragha, kurahisisha utendekaji wa shughuli za sanaa za maonyesho pamoja na zile zilizo nje ya sanaa za maonyesho pamoja na kujenga tabia za kuthaminiana miongoni mwa wanajamii.

Marejeleo

- Bakhressa, S. K. (1992). *Kamusi ya Maana na Matumizi*. Dar es Salaam: Oxford Univesity Press.
- Banham, M. (Mhariri) (2004). *A History of Theatre in Africa*. New York: Cambridge University Press.
- Chuachua, R. (2010). "Suala la Itikadi katika Riwaya za Shaaban Robert". Tasnifu ya Shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Chuachua, R. (2016). "Falsafa ya Riwaya za Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi katika Muktaba wa Epistemolojia ya Kibantu". Tasnifu ya Shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa).
- Conteh-Morgan, J. (2004). Francophone Africa south of the Sahara katika *A History of Theatre in Africa*. Martin Banham (Mh.). New York: Cambridge University Press.
- Ebner, P. E. (2012). *Wangoni: Vita, Hadithi, Methali na Vitendawili*. Songea: Ndanda-Peramiho Press.
- Ebner, P. E. (2009). *The History of the Wangoni*. Songea: Peramiho Printing Press.
- Fustine, S. (2017). "Usawiri wa Falsafa ya Kiafrika na Mchango Wake katika Ujenzi wa Mtindo wa Uhalisiajabu Katika Riwaya ya Kiswahili: Mifano Kutoka katika Riwaya Teule za Kiswahili za Kihalisiajabu". Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu katika Fasihi ya Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa).
- Kiango, S. D. (1973). "Maendeleo ya Fasihi ya Kiswahili Upande wa Michezo ya Kuigiza", katika *Kiswahili*, TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Toleo la 43, Na. 2, Uk. 88 - 96
- Mbiti, J. S. (1969). *African Religion and Philisophy*. London: Morrison and Gibb Ltd.
- Mbogo, E. (1993). "Matumizi ya Dhana na Sanaa za Maonyesho za Jadi katika Tamthiliya za Leo" katika *Fasihi, Uandishi na Uchapishaji*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Milinga, G. (2016). *Mwenge*, ISSN 0856 - 0722 Reg. Nb 15, Toleo la 931, 'Makabila Yaliyoishi Nchi ya Ungoni Kabla ya Ujio wa Wangoni Toka Afrika ya Kusini', Juni 2016.
- Ponera, A.S. (2014). *Utangulizi wa Nadharia ya Fasihi Linganishi*. Dar es Salaam: Karljamer Print Technology.
- Sengo, T. S. Y. (1995). "Itikadi katika Jamii za Kiswahili", katika *Lugha, Utamaduni na Fasihi Simulizi*, TUKI, Dar es Salaam uk. 27 – 40.

- Simchimba, E. A. (2012). "Falsafa ya Kiafrika katika Methali za Kiswahili". Tasnifu ya Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijchapishwa).
- Tempels, P. (1959). *Bantu Philosophy*. Paris: Presence Africaine.
- TUKI. (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

